JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS – TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA ARUSHA

SHULE YA SEKONDARI MRINGA,
S. L. P. 7188,
ARUSHA.

TAREHE _____

NAMBA YA MKUU WA SHULE: 0754 507 888
NAMBA YA MAKAMU WA SHULE: ***0754 504 209***

Kumb. Na. MSS/ADM/VOL.12/017

JINA……..

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO MWAKA 2018

Ninayo furaha kukujulisha kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha Tano katika shule hii mwaka 2018, tahasusi ya …..... Shule ya Sekondari Mringa ipo umbali wa kilometa 8 kutoka Arusha Mjini. Usafiri wa basi kutoka mjini Arusha unapatikana Standi Ndogo na nauli ni Tshs. 450/=.

1. Shule hii ni ya bweni kwa wasichana pekee kuanzia kidato cha kwanza hadi cha sita.
2. Unatakiwa kufika shuleni tarehe 17/07/2018 bila kukosa wala kuchelewa tayari kuanza masomo ya kidato cha TANO. Muhula wa masomo unaanza tarehe 17/07/2018. Mwisho wa kuripoti ni tarehe 04/08/2018.
3. Muda wa kuripoti ni kabla ya saa kumi na mbili jioni, baada ya muda huo hautapokelewa.
4. Karo (ADA) ni Tsh. 35,000/= kwa muhula na Tsh. 70,000/= kwa mwaka. Ada hii ni muhimu ilipwe kwenye akaunti ya shule iliyoko **NMB Clock Tower 40801200228,** akaunt hii ni kwa ajili ya **ada** tu.

N.B: Pesa hazitapokelewa shuleni.

5. Njoo na pay in slip ya Benki kwa uthibitisho wa malipo hayo.
6. Njoo na slip ya matokeo yako ya kidato cha nne.

MICHANGO MINGINE ILIPWE BANK YA NMB AKAUNTI NA. 40801200048.

I. Tahadhari Tsh. 5,000/= (hairudishwi)
II. Kitambulisho Tsh. 6,000/=
III. Mchango wa wahudumu (walinzi, karani, mkutubi, wapishi) Tsh. 30,000/=
IV. Taaluma Tsh. 20,000/=
V. Nembo ya shule Tsh. 2,000/=
VI. Matibabu Tsh. 10,000/= (Huduma ya kwanza na Bima ya Afya)
VII. Ukarabati wa samani Tshs. 15,000/=.
VIII. Mitihani ya kujipima Tshs. 20,000/=

SARE YA SHULE

I. Blauzi nyeupe mbili (2) za mikono mifupi na zisizo na urembo wowote.

II. Sketi mbili rangi za kijivu iliyokolea, kitambaa cha sketi kinapatikana shuleni kwa Tsh. 14,000/= kila moja.

III. Sweta rangi nyeusi (Kenya) na sweta isiyo na mikono (kisibau) pia zinapatikana shuleni kwa Tsh. 17,000/= kila moja.

IV. Viatu vya ngozi vyeusi vya kamba visivyo na visigino virefu.

V. Tai nyeusi yenye mistari myeupe, pia zinapatikana shuleni kwa Tsh. 3,000/=

VI. Stocking nyeupe.

MAHITAJI MENGINE YA SHULE

I. Rim moja (1) ya karatasi za photocopy.

II. Nguo za michezo, raba nyeusi, sketi fupi ya blue bahari (nap round) bukta blue bahari na T-shirt nyeupe.

III. Track suit ya dark blue – zisizobana.

IV. Shamba dress gauni Ia dark blue, pia linapatikana shuleni kwa Tsh. 15,000/= kila moja.

V. Godoro Ia futi 2 ½ na neti

VI. Shuka mbili rangi ya blue.

VII. Blanketi moja (1).

VIII. Mto na foronya.

IX. Nguo za kulalia.

X. Sanduku Ia chuma lenye kufuli imara kwa ajili ya kuhifadhia vifaa vyako.

XI. Bakuli, sahani na kijiko (visiwe vya udongo).

XII. Ndoo lita 20; Hard broom 1; rubber squeezer 1 kwa ajili ya usafi.

XIII. Madaftari ya kutosha (counter books).

XIV. Scientific calculator na mathematical set.

VITABU:

Ifuatayo ni orodha ya vitabu vinavyotumika darasani. Mwanafunzi ajitahidi kuwa navyo angalau baadhi.

I. **ECONOMICS**

- Text book of economics: By J. I Hanson
- Economics simplified: By Saleemi
- Modern Economics: By Khan

II. **MATHEMATICS**

- Pure Mathematics - K. J Backhouse
- Advanced level mathematics - L.K. Shayo.

III.

IV. **GEOGRAPHY**

- Landforms in Africa: By Colin Buckle
- Principles of Physical Geography: By Monk house
- Geography intergrated approch: By Waugh
- Practical Geography for Africa: By J. M Pritchard
- Africa: By J. M. Pritchard
- Tropical lands: By Michael Seniar.
- Human and Economic Geography: By Morgan.

v.

VI. **ENGLISH LANGUAGE**

- A Man of the people - Chinuo Achebe
- The Beautiful Ones are not yet born - Ayi Kwei Amar
- An Enemy of the people - Hendrick Ibsen
- Betrayal in the city - Francis Lubuga
- Selected poems -Tanzania Institute of Education
- The wonderful surgeon and other poems - C. Mloka
- Advanced Level English, A practical approach - Nicholaus Asheli

VII. **HISTORY BOOKS:**

- History of Africa – By Kelvin Shilington
- History Paper 2 Notes Advanced Level Form 5 & 6 By Gervas M. Zombwe
- Mastering Advanced Level History Book One – By Mwl. Kato A. Kassim.
- Focus on Modern World History – By Jophace Poncian
- Advanced Learning History Form 5 And 6 - By Oxford.

VIII. **ACCOUNTANCY BOOKS:**

- Financial Accounting - By (i) R. L. Gupta

(ii) V. K. Gupta

- Business Accounting 2 (eight Edition) - By (i) Frank Wood
  (ii) Jangster
- Simplified Accounting – By N. A. Jaleemi

IX. **COMMERCE BOOKS:**

- Commerce by Mubiru Musa
- Commerce by C. R. Rwabutoga
- Commerce Simplified For East Africa – N. A. Saleemi
- Advance Level Commerce – by C. M. Ambilikile.

……..…

C. KAHANGWA

MKUU WA SHULE

MASHARTI YA KUZINGATIA WANAFUNZI WOTE WA BWENI

1. Wanafunzi wale waingiao bweni wanapaswa kufuata masharti yote ya shule.
2. Usafi wa bweni ni wajibu wa kila mwanafunzi anayeishi kwenye bweni.
3. Kila rnwanafunzi aheshimu kazi ya mikono zote mbili ikiwa ni pamoja na bustani za maua, usafi wa mazingira na anapaswa kuheshimu masorno ya darasani.
4. Kila mwanafunzi aheshimu na kutunza mali ya shule, uharibifu wowote utakaotokea ndani ya bweni itabidi ugharamiwe na mwanafunzi mwenyewe.
5. Ugomvi wa maneno, matusi, kupigana ni mwiko.
6. Ruhusa zote za kulala nje ya shule zitatolewa na Mkuu wa shule au Makarnu wake tu.
7. Ni lazima kuzima taa saa 4:00 usiku na kulala,
8. Mwanafunzi hatakiwi kubaki bweni wakati wa masomo bila taarifa au ruhusa ya mwalimu wa zamu au matron.
9. Kelele zisizo na rnaana ni mwiko ndani ya bweni.
10. Mwanafunzi yeyote haruhusiwi kutumia vyombo vya umeme kama vile heater, radio, pasi ya umeme, jiko ndani ya bweni au kufanya ufundi wa aina yoyote kwenye umeme ndani ya bweni na darasani.
11. Mwanafunzi yeyote haruhusiwi kwenda nyumbani kwa mwalirnu au mfanyakazi asiye mwalirnu bila ruhusa.
12. Ni marufuku mwanafunzi kuwa na vifaa vyenye ncha kali au vitu vinavyolipuka na dawa za aina zozote ndani ya bweni.
13. Ni marufuku kwa mwanafunzi wa bweni kubaki ndani ya bweni au kuzurura nje wakati wa preparation (saa 2:00 usiku — 4:00 usiku).
14. Siku ya kutembelea wanafunzi wa bweni ni jumamosi ya kwanza ya rnwezi kuanzia saa 7 mchana mpaka 10:00 jioni na wageni wote wataingia ofisi ya mwalimu wa zamu.

(A) MAVAZI

I. Nguo za binafsi haziruhusiwi shuleni.

II. Wanafunzi wote wa bweni wanatakiwa muda wote wavae sare za shule (shamba dress) baada ya masomo hawaruhusiwi kuvaa nguo nyingine tofauti na sare zinazotakiwa. Nguo zote ni lazima ziwe ndefu chini ya magoti na mabega yasiwe wazi.

III. Wanafunzi wa bweni wanatakiwa wawe na mashuka mawili ya blue yasio na maua (plain) blanketi 1) mto 1, godoro na sanduku 1 Ia bati.

(B) CHAKULA

I. Wanafunzi wa bweni watapata chakula cha kawaida kufuatana na kiwango cha fedha kinacholipwa.

II. Wanafunzi wote wanatakiwa wawe na sahani 1, bakuli 1, kikornbe, kijiko 1 (viwe vya udongo).

(C) MATIBABU

Taratibu za hudurna ya kwanza zitapangwa na Mkuu wa shule pindi mwanao atakapojiunga na bweni aidha endapo mwanafunzi ataugua mzazi atagharamia matibabu.

SAINI YA MWANAFUNZI…….. TAREHE……..

SAINI YA MZAZI / MLEZI …… TAREHE ……..

SHERIA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye Dhamana ya Elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

a. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazirna.

b. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule.

c. Ni muhimu kutimiza kwa makini maandalio ya jioni (preparation)

d. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine.Utakazopewa.

e. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.

f. Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule.

g. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.

h. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.

MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA UKAFUKUZWA SHULE

1. Wizi
2. Kutokuhudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro
3. Kugoma na kuhamasisha mgomo
4. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla.
5. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule.
6. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya.
7. Uvutaji wa sigara
8. Uasherati, uhusiano wa jinsi moja.
9. Kupata ujauzito au kutoa mimba
10. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
11. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
12. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
13. Kudharau bendera ya Taifa.
14. Kufanya jaribio lolote la kujiua au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.
15. Uharibifu wa mali ya Umma kwa makusudi.
16. Kuwa na simu shuleni.

SHULE YA SEKONDARI MRINGA

FOMU YA KUKUBALI NAFASI NA UTII

Mimi…….. . (Jina kamili)

Kidato cha……. mwaka …….

Nakubali na naahidi kufuata sheria na Taratibu za shule kama zilivyopangwa. Nikienda kinyume nichukuliwe hatua za nidhamu.

TAREHE…… **……**

JINA NA SAINI YA MWANAFUNZI

Mimi mzazi /Mlezi wa …….

Nimesoma na kuelewa /kukubaliana na sheria na kanuni za shule. Endapo mtoto wangu atashindwa kufuata hayo yote hatua kali dhidi yake zichukuliwe ikiwa ni parnoja na kusimamishwa masorno.

TAREHE …… **……**

JINA NA SAINI YA MZAZI / MLEZI

KUMBUKA: SHULE YETU WASICHANA **HAWASUKI NYWELE** TAFADHALI KUBALIANA NALO KABLA YA KUSAINI FOMU YA KUKUBALI NAFASI ULIYOPEWA YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MRINGA.

SHULE *YA* SEKONDARI MRINGA

FOMU YA KUJIANDIKISHA SHULENI

HABARI ZA MZAZI / MLEZI

1. Jina kamili Ia Baba ……..
2. Kazi yake……
3. Jina kamili la Mama…….……..
4. Kazi yake…….……
5. Jina kamili Ia Mlezi (iwapo mtoto haishi na wazazi wake) ……..
6. Kazi na anwani ya mIezi ……....
7. Nyumbani kwa Baba (alipozaliwa mtoto) au Place of Domile Kijiji /Mtaa ……..…..Wilaya……..……. Tarafa …….
8. Anwani ya mahali pa kazi ya baba…….. Namba ya simu……
9. Anwani ya mahali pa kazi ya mama……... Namba ya simu…….
10. Mtoto anaishi na (I) Baba tu (ii) Mama tu (iii) Wazazi wote (iv) Walezi (Kata isiyohusika)

TAREHE…….. ……

JINA NA SAINI YA MZAZI / MLEZI

MRINGA SECONDARY SCHOOL

REQUEST FORM FOR MEDICAL EXAMINATIONS

FROM. …….

……...

……

DATE…….

MR. /MRS /MISS……

Please examine the above named as to his/her physical and mental fitness for a full time student in Secondary school. The examination should include the following categories:-

1. (a) Eye sight (b) Hearing (c) Limbs
   (d) Speech (e) Venereal Diseases (f) Leprosy
   (g) Epilepsy
2. Neurosis
3. Other serious Disease
4. Pregnancy

MEDICAL CERTIFICATE

(To be completed by a Government Medical Officer)

5. (a) Eye – sight
   (b) Hearing
   (c) Limbs
   (d) Speech
   (e) Venereal Diseases
   (f) Leprosy
   (g) V- Neuroses
   (h) Other serious diseases
   (i) Pregnancy

Date:……Signature ……

Station …… Destination ……

(Delete as necessary)